

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Simu Nambari: 2152532/3  
Baruapepe: [cg@dcea.go.tz](mailto:cg@dcea.go.tz)  
Tovuti: [www.dcea.go.tz](http://www.dcea.go.tz)  
Nukushi: 2152820



8Barabara ya kivukoni  
S.L.P. 80327  
Dar es Salaam  
Tanzania

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

#### MAMLAKA YAZINDUA KITUO CHA MUDA CHA KUTOLEA TIBA YA METHADONE KWA WAATHIRIKA WA DAWA ZA KULEVYA KATIKA HOSPITALI YA BOMBO MKOANI TANGA

**Tanga, 24 Juni 2020:**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imezindua kituo cha muda cha kutoa huduma ya Methadone kwa waraibu wa dawa za kulevya aina ya heroin. Kituo hicho kimezinduliwa leo tarehe 24 Juni, 2020 na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Umyy Mwalimu katika hospitali ya Bombo mkoani Tanga.

Kwa kutambua umuhimu wa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya Serikali imezindua kituo hiki cha muda ikiwa ni katika kutekeleza wa mpango wake wa muda mfupi ili kuweza kufikisha huduma kwa walengwa kwa haraka. Aidha uanzishwaji wa kituo hiki umetokana na tafiti zilizofanyika ambazo zimeonesha mkoa wa Tanga kuwa ni moja ya mikoa iliyoathirika na matumizi ya dawa za kulevya. Serikali katika mpango wake wa muda mrefu inaendelea na taratibu za ujenzi wa kituo cha kudumu ambacho kitakuwa kikubwa na chenye uwezo wa kutoa huduma kwa wathirika wengi zaidi.

Uzinduzi wa kituo hiki ni muendelezo wa vituo vingine vilivyopo Nchini, kwani mpaka sasa kuna vituo nane (8) ambavyo vinatoa huduma kila siku kwa waraibu wapatao 8,500. Katika vituo hivyo, vitatu vipo katika jiji la Dar es Salaam katika Hospitali za Rufaa Mwananyamala, Muhimbili na Temeke, mkoani Mbeya katika Hospitali ya Rufaa ya

Nyanda za Juu Kusini, mkoani Mwanza katika Hospitali ya Rufaa ya Sekou Toure, mkoani Pwani eneo la Bagamoyo na Itega jijini Dodoma.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaratibu uendeshaji wa vituo hivi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Serikali kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inatoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Tanga kushirikiana na asasi na wadau wengine katika kuwashawishi waathirika wa dawa za kulevya waweze kufika kwenye kituo hicho kupata huduma za tiba na ushauri.

**Imetolewa na,**



Florence Khambi

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA.**